MAPAMBANO YA UMMA DHIDI YA MBINU ZA KINYANYASAJI NA UKANDAMIZAJI[♣]

Profesa Chachage Seithy L. Chachage
Idara ya Sosholojia
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Maelezo ya Awali

Mnamo wiki za mwisho za mwezi Julai mwaka 1905, wazalendo wa kusini mwa Tanzania, kuanzia Umatumbini, walianzisha vita dhidi ya mkoloni wa Kijerumani—ita vya ukombozi vya Maji Maji. Vita hivyo vilianza mara baada ya wazalendo wa Nandete kung'oa mimea ya pamba ambayo ilikuwa imeshaanza kukomaa. Kitendo hiki kilikuwa ni ishara ya wazi ya chuki ambayo Waafrika walikuwa nayo dhidi ya utawala wa kikoloni; na pia kilikuwa wito wa kuwataka Waafrika waanze vita vita dhidi ya utawala huo. Nchi ilikuwa imetawaliwa na Wajerumani tangu mwaka 1885; na kuanzia mwaka 1888 kulikuwa kumetapakaa mapambano dhidi ya madhalimu hao karibia nchi nzima. Na ni haya mapambano yaliyokuwa yameanzishwa na akina Mkwawa, Bwana Heri, Machemba, Siki na wengineo ndiyo hatimaye yaliyopelekea kwenye hivi vita dhidi ya tamalaki ya Mjerumani mwaka 1905 vilivyoongozwa na Kinjeketile Ngware. Na katika mwaka huo huo mapambano dhidi ya utawala wa Kijerumani yalitokea huko Namibia na Kameruni.

Babu na bibi zetu walisimama kidete dhidi ya ukandamizaji, unyonyaji, uporajwi wa ardhi, ushurutishwaji kuajiriwa na masetla na makampuni ya mashamba makubwa (plantations) ya Wazungu kwa ujira duni, ulazimishwaji kuzalisha bidhaa za kuwanufaisha wakoloni, kulipishwa kodi ya kuuhimili utawala wa kikoloni na wanyonyaji wengine, na mengineyo mengi ya kidhalimu. Baada ya Tanganyika African National Union (TANU) kuanzishwa mwezi Julai 1954, watu wa kwanza kuipokea TANU kwa wingi kufikia mwaka 1955, walikuwa ni wale wale wa Umatumbi na Ungindo, ambako vita vya Maji Maji vilianzia. Wangindo walitamka wazi kwamba Nyerere alikuwa Kinjeketile mwingine; ni mzimu wa Hongo uliokuwa umerejea na wakatilia shaka msimamo wa Nyerere uliodai kuwa iliwezekana kuwaondoa wakoloni kwa njia ya amani bila silaha (Illife 1979: 520).

Wakati akitoa utetezi wake wa haja ya Tanganyika (kama ilivyojulikana wakati huo) kupata uhuru kwenye Umoja wa Mataifa huko New York mnamo mwaka 1956 (miaka 51 baada ya vita hivyo), Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikumbushia mapambano haya. Aliwaambia wajumbe wa mkutano huo kwamba katika vita hivyo, watu wa Tanganyika walikuwa wamepigana kwa mikuki, mishale, virungu, visu na mapanga yenye kutu dhidi ya utawala wa Wajerumani tangu waingiliwe. Alikumbusha kwamba katika majaribio yote hayo

[♣] Mada kwa ajili ya "Kongamano juu ya Harakati za Wanyonge Dhidi ya Michakato ya Sera za Ufukarishaji", lililoandaliwa na Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), na kufanyika tarehe 12 hadi tarehe 13 Mei 2005, katika ukumbi Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC), Kurasini, Dar es Salaam.

Waafrika walishindwa kuwaondoa wakoloni na jaribio la mwisho likawa ni hivyo vita vya Maji Maji, ambavyo kutokana na ukatili na uuaji wa Wajerumani vilisababbisha vifo vya zaidi ya watu 120,000. Akatamka wazi kwamba, katika mapambano ya miaka yote hiyo, hakukuwa na wachochezi wa kizalendo au watu waliobobea katika masuala ya umagharibi au Makomunisti waliosababisha wananchi kuwapinga Wajerumani. Bali, "Wananchi walipambana kwa sababu walikuwa hawaamini kwamba watu weupe walikuwa na haki ya kuwatawala na kuwastaarabisha watu weusi. Walianzisha vita hivyo vya kishujaa siyo kwa sababu ya uoga wa vuguvugu la kigaidi au kiapo cha kishirikina, bali kwa kuitikia mwito wa kimaumbile, mwito wa imani ambao umejikita katika mioyo ya binadamu wote na kwa nyakati zote, miongoni mwa waliosoma na wale ambao hawakusoma, wa kuasi dhidi ya utawala wa wageni. Ni muhimu kulizingatia akilini hili,..."[1]

Nimeanzia na maelezo hayo kama utangulizi wa makala yangu kwa sababu, huu mwaka wa kukitathmini mwelekeo wa mapambano ya utetezi wa haki za wazalishaji wadogo wadogo za HAKIARDHI, pia ni mwaka wa 100 wa maadhimisho ya mwanzo wa vita vya Maji Maji ambavyo vilidumu hadi mwaka 1907. Kadhalika, inakaribia miaka 20 tangu watawala wa Tanzania waingie katika mikataba ya kutekeleza masharti ya nchi za Magharibi ambayo ni ya kidhalimu na yamelenga yakuyaimarisha mahusiano ambayo wahenga wetu waliyakana kwa nguvu zote. Masharti hayo yanayosimamiwa na Benki ya Dunia, Shirika la Kimataifa la Fedha, Shirika la Biashara la Dunia na taasisi zingine za kifedha za nchi za magharibi. Ni kwa sababu hii watawala wetu wamesahau kabisa umuhimu wa maadhimisho haya ya vita vitukufu vya Maji Maji. Wamesahau kwamba huu ulikuwa uwe mwaka wa tafakuri na tathmini ya mapambano ya Waafrika dhidi ya udhalimu wa kila aina na kujifunza yanayoweza kutusaidia kutokana na historia hiyo.

Ilibidi mwaka huu Watanzania tusimame kidete na kuwadai kwa nguvu zote Wajerumani na wakoloni wengine walipe fidia kwa maovu na udhalimu wao, kama ambavyo Japan na nchi zingine za kidhalimu zililazimika kulipa fidia kutokana na maovu ziliyoyatenda. Laiti kama hao wahenga wangalifufuka leo na kuwasikia wajukuu wakiusifia ubeberu na ukoloni mambo leo kwa kuuremba kwamba ni utandawazi; wakawapamba wanyonyaji kwamba ni wawekezaji au wabia katika maendeleo; wakaugeuza ushurutishwaji kuwa ni ushirikishwaji; na kisha wakiwaita wanaosimamia hayo mahusiano wafadhili au marafiki zetu; bila shaka wangekana na kulaani kwamba huu sio uzao wao!

Ukweli ni kwamba ukoloni na ukoloni mamboleo daima umelenga kujenga mahusiano ya kinyonyaji yaliyojikita katika uporaji wa ardhi na raslimali, ulazimishaji wa wazalishaji kuzalisha mali na bidhaa za kukidhi mahitaji ya watu wa magharibi na uwepo wa

[1] Tafsiri ya kwangu. Maneno yake mwenyewe: "The people fought because they did not believe in the white man's right to govern and civilize the black. They rose in a great rebellion not through fear of a terrorist movement or a superstitious oath, but in response to a natural call, a call of the spirit, ringing in the hearts of all men, and all times, educated or uneducated, to rebel against foreign domination. It is important to bear this in mind,…" (Nyerere 1966: 41)

soko la wafanyakazi wa ujira duni. Maana halisi ya ujenzi wa mahusiano kama hayo ni ujenzi wa matabaka miongoni mwa mataifa na ndani ya mataifa (matabaka ya wanyonyaji na wanyonywaji, madhalimu na wadhulumiwao, wagandamizaji na wagandamizwaji, wasiozalisha na wazalishaji, wawekezaji na wawekezwao, wenye nguvu na mabavu na wanyonge, wafadhili na wafadhiki, n.k.) na ubaguzi na utengwaji kirangi, kikabila, kijinsia na hata kirika na kinasaba. Mapambano ya umma kwa ujumla siku zote yamekuwa dhidi ya mfumo kama huo, kwa nia ya kujenga jumuia ya kibinadamu iliyojikita katika mahusiano ya misingi ya usawa, heshima, uhuru na haki za kijamii kwa ujumla. Hivi leo, kwa wale waliokubuhu katika fikra za kimagharibi, matamanio ya ujenzi wa jumuia kama hiyo ni ndoto za wajukuu wa Alinacha na ni za kukejeliwa na kukebehiwa!

Mapambano ya wanyonge dhidi ya ufukarishwaji ni mada pana sana, kwani miongoni mwa wanyonge hao kuna wafanyakazi, wakulima, wafugaji, wavuvi, wachimbaji madini wadogo wadogo, wafanya biashara wadogo na wazalishaji wa bidhaa wadogo, na makundi mengine. na Haya ni mambo mengi kuyaelezea na kuyamaliza yote katika makala fupi kama hii. Kitakachofanyika katika makala hii ni kuyavinjari kwa ujumla kwa kukumbushia historia ya mapambano ya watu wa makondeni (wakulima) tu, katika kupigania kulinda ardhi na raslimali zao, kwa kusudi la kuutafakari muktadha wa mapambano ya leo na mwelekeo wake. Husemekana kwamba historia hujirudia kwa wale wasiotaka kuzingatia mafunzo yake; na pindi ikifanya hivyo hatima yake huwa tanzia. Katika hali kama hiyo kwa wale ambao wameidharau, yenyewe hubaki ikijifaragua na kuwakodolea macho huku ikiwacheka kwa ujinga na uzembe wao.

Harakati za Wakulima na Mwamko wa Kitaifa

Chini ya ukoloni wa Kijerumani (1885-1916) ni masetla na makampuni ya mashamba makubwa tu ndiyo yalikuwa na haki ya kumiliki ardhi kisheria kwa kutunzwa hati. Waafrika walikuwa na haki ya kuitumia ardhi, na sio kumiliki, kwani ardhi yote ya nchi ilimilikiwa na dola ya kikoloni. Misingi ya sera za Wajerumani ilikuwa ni ujenzi wa uchumi wa kisetla na makampuni ya mashamba makubwa. Hivyo basi, hadi kufikia mwaka 1914 Wajerumani walikuwa wamepora ekari 1,300,000 za ardhi yenye neema kiuzalishaji kaskazini mwa nchi na upande wa pwani kwa ajili ya kuwamilikisha wageni. Idadi ya Wazungu iliongezeka nchini kutoka 1,390 hadi 4,998 kati ya mwaka 1904 na 1913, na kati ya hao, 882 walikuwa wakijishughulisha na kilimo. Idadi hii ilikaribia kuwa sawa na ile ya masetla waliokuwepo Kenya wakati huo (Illife 1979: 141).

Wakoloni walipora pia maeneo mengine makubwa kwa ajili ya hifadhi za misitu na wanyama kwa kisingizio cha kuhifadhi mazingira. Kulikuwa na maeneo manane yaliyotengwa kwa ajili ya wanyama pori hadi kufikia mwaka 1908. Kabla tu ya Vita vya Kibeberu vya Kwanza vya Dunia vilivyoanza mwaka 1914, idadi ya maeneo haya ilifikia 11. Mnamo miaka ya

1920, Waingereza waliyapanua zaidi maeneo haya na idadi yake ikafikia 13 (maili za mraba 16,300). Katika kuanzisha na kuyapanua maeneo haya, watu waliondolewa na kuhamishwa kwa nguvu. Hivi ndivyo watu wa maeneo ya Lindi, Wamasai, watu wa Rukwa, wale wa Gombe, na kwingineko walivyopoteza ardhi zao. Uporaji wa ardhi kwa ujumla ulikuwa ni njia ya wakoloni ya kuwalazimisha wenyeji waingie katika kazi ya ujira kama njia pekee ya kujikimu na kulipa kodi kutokana na kunyang'anywa nyenzo za aina yote za uzalishaji. Ulipishaji kodi ulianzishwa mahsusi kama njia ya kuwalazimisha iliyowalazimisha wenyeji ambao hawakuporwa ardhi kuzalisha bidhaa za kuuza nje ili wapate fedha za kulipia kodi na pia kuingia katika mahusiano ya uzalishaji wa bidhaa badala ya ule wa kujikimu.

Uporaji wa kasi wa ardhi ulikuwa umefanyika kabla ya vita vya Maji Maji. Baada ya vita hivyo, kasi hiyo ilipungua kidogo, na kadhalika ulazimishaji watu kuwa manamba ulifanyika kwa uangalifu zaidi. Wakoloni wakabuni mbinu walizoiita "ukoloni wa kisayansi" (scientific colonialism), ambao ulizingatia malengo ya ukoloni ya kujinufaisha bila ulazima wa kuwanyang'anya ardhi wenyeji. Hadi hapo walikuwa wamefikia uamuzi kwamba iliwezekana kabisa kuwafanya wazalishaji wadogo—wakulima—kuzalisha vilivyohitajika na nchi za magharibi, kwani mfumo wa ulipaji wa kodi ungewalazimisha kuzalisha mazao ya biashara (Gann & Duignan 1977: 75). Waingereza waliifahamu fika hii historia ya wenyeji kupigana dhidi ya wakoloni; hivyo mwanzoni walikuwa waangalifu sana katika mipango yao ya kupora ardhi.

Kuondoka kwa masetla na makabaila wa mashamba makubwa wa Kijerumani pia kuliwezesha Waingereza kutovamia ardhi zaidi kwa muda mfupi, kwani masetla wa Kiingereza na wengine walioingia wakati huo walirithishwa na kulimilikishwa mashamba hayo. Waingereza walikuwa na hofu wakati huo kutokana na hali waliyoikuta katika nchi hili wakati huo: waliwakuta wenyeji ambao walikuwa hawawaamini Wazungu na sera zao za aina yoyote ile, na hasa zile zilizohusu masuala ya ardhi. Hivyo Waingereza walilazimika kuendelea na sera za Wajerumani za kabla ya Vita vya Kibeberu vya Pili vya Dunia, wakaanzisha hata utawala wa kikabila[2]—wa machifu hata kule ambako hawakuwahi kuwepo kihistoria—wa kusimamia maslahi ya kikoloni (utawala wa wenyeji—indirect rule), kama njia ya kuepusha shari, kwa kisingizio kwamba wao walikuwa wamekuja nchini kuwaendeleza wenyeji.

[2] Historia inatudhihirishia kwamba, makabila, kama yafahamikavyo leo yalianzishwa na wakoloni. Jumuia nyingi hapa nchini hazikuwa na machifu—Wazaramo, Wangindo, Wasukuma, Wazanaki, Wabena, Wamaasai, n.k. Himaya chache zenye machifu zilikuwa zimeanza kuibuka katika miaka ya 1860, na si kabla ya hapo. Nazo hizo ni kama zile za akina Mkwawa, Merere, Mbega, Siki, Machemba, n.k. Enzi hizo Wanyamwezi maana yake ilikuwa ni watu watokao magharibi, Wasukuma ni watu watokao kaskazini, Wasambaa ni watu watokao milimani, Wabondei ni watu watokao mabondeni, n.k. Kilichowatambulisha ni eneo la kijiografia walikotokea au shughuli walizozifanya, na siyo uanajamii wao kisiasa kama ilivyo leo. Kwa ujumla watu walikuwa ni wamoja, na kilichofanyika na wakoloni ni kuwagawa ili kuwepo uwezekano wa kuwatawala (divide and rule). Historia ya mahusiano ya utani hapa nchini—kati ya wazaramo au Wakwere na wasukuma au Wanyamwezi, na watu wa sehemu zingine unatokana na haya mahusiano ya umoja yaliyokuwepo, ambayo msingi wake ulikuwa ni kutegemeana, kwani ilibidi Wakerewe wasafiri hadi ufipa au Ukinga kupata majembe na wengine ilibidi waende hadi Pwani kutafuta chumvi. Utani uliotokana na vita ni ule wa Wngoni ambao walikuwa wamewakimbia makaburu Afrika ya Kusini, wakaja huku kutafuta maeneo ya kuishi miaka ya 1860 na ule wa Wamaasai na majirani zao ambao ulikuwa ni wa kuibiana ng'ombe!

Katika kuanzisha utawala wa wenyeji, Wazungu walidai kwamba walikuwa wanarudishia taasisi za utawala za kiasili, ambazo kwa hoja yao, zilikuwa zimevurugwa na Wajerumani. Walidai kwamba asili ya Waafrika ni kutawaliwa na machifu na kuishi katika vijiji chini ya mfumo wa ujima. Kwa hiyo basi, umiliki wa ardhi wa Waafrika ulikuwa kimsingi wa ujima. Kwa sababu hiyo, wakaanza kuwakusanya wenyeji kwa nguvu na kuwalazimisha kuishi katika vijiji kuanzia miaka ya 1920 kwa visingizio hivyo. Hivyo ndivyo walivyowafanyia wenyeji wa sehemu zote za magharibi mwa Tanganyika, huko Lindi na sehemu nyingine nyingi za nchi hii, wakati mwingine wakisingizia kwamba nia yao ilikuwa ni kuondoa matatizo ya ueneaji wa ugonjwa wa malale kwa kutokomeza mbung'o na kuwaletea watu maendeleo (kwa kuwepatia huduma za afya, ushauri, elimu, masoko, n.k.). Sababu za msingi za vitendo hivyo zilikuwa ni uwezekano wa kuwatawala na kuwagandamiza wenyeji kirahisi, kwani watu wakiwa pamoja ilikuwa rahisi kusimika mtawala, kukusanya kodi, kuwakamata wakawe manamba, kuwashurutisha kulima mazao yaliyohitajika na wakoloni na kuyakusanya kirahisi, n.k. (Kjeshus 1977).

Kipindi cha miaka ya 1920 hadi 1940 kilikuwa ni kipindi cha wasiwasi mkubwa miongoni mwa wenyeji kutokana na matendo hayo ya Wakoloni kuwaondoa katika maeneo ya makazi na shughuli zao na kuwakusanya katika vijiji. Kwa sababu hiyo, wenyeji waliasi mara kwa mara dhidi ya mipango ya aina yoyote ile iliyobuniwa na wakoloni kwa kisingizio chochote kile—iwe utunzaji wa mazingira, kulima pamba,[3] kuzuia mmomonyoko wa udongo au hata huo utawala wa kienyeji na hao machifu. Waliwapinga pia wafanya biashara wa Kihindi ambao walinunua mazao yao kwa bei hafifu. Uasi huo mara nyingine ulifikia hatua ya kutumia nguvu ikiwa ni pamoja na silaha. Kwa mfano, kulitokea vurugu kubwa sana dhidi ya utawala wa wenyeji (native authorities) na vyama vya ushirika mnamo mwaka 1937 huko Bukoba na Kilimanjaro baada ya serikali kutoa rasimu ya masharti ya upandaji kahawa. Wakulima walihisi kwamba masharti hayo yalikusudia kuwafukarisha wale ambao walikuwa pembezoni hadi wakashindwa kuzalisha, kwani yaliwataka wasipande migomba na mazao mengine ya chakula katika mashamba ya mibuni. Kutokana na vurugu hizi, wenyeji kadhaa walifungwa (Coulson 1982: 64).

Wasukuma, ambao ardhi zao hazikupata kunyanga'anywa walipinga kwa mabavu mpango wa wakoloni wa kuwataka wabadilishe mfumo wa kilimo na ufugaji kuanzia mwaka 1946 (Maguire 1969). Wapare waligomea kodi na mipango ya kuwataka wabadilishe mfumo wa kilimo (Kimambo 1971); kadhalika, kulikuwa na maasi huko Usambara, Singida, Mbulu, Iringa, Uluguru na kwingineko, dhidi ya hiyo mipango ya kubadilisha mfumo wa kilimo na ufugaji. Hatima ya maasi haya ilikuwa ni kuudhofisha utawala wa machifu ambao ulikuwa umesimikwa na wakoloni na ulisimamia maslahi ya wakoloni hao hao. Hawa watu wa makondeni walikuwa

[3] Sote tunayafahamu masimulizi yanayohusu ukaangaji wa mbegu za pamba kabla ya kuzipanda au kupanda mhogo shina likiwa juu. Hizo zilikuwa ni baadhi ya mbinu za mapambano ambayo yalichukua sura za aina nyingi.

sahihi kabisa kuasi na kufanya vurugu, kwani baada ya Vita vya Pili vya Kibeberu vya Dunia Waingereza walitupilia mbali visingizio vyote vya awali vya kutowaingilia wenyeji katika masuala ya ardhi na kuanza kupora maeneo makubwa ya ardhi kwa ajili ya kuwaleta masetla ambao wangeongeza uzalishaji haraka ili kulipia madeni ya yaliyotokana na Vita vya Kibeberu vya Pili vya Dunia kwa Wamarekani na kuujenga upya uchumi wa Uingereza ambao ulikuwa umeharibika vibaya sana kutokana na vita hivyo. Wazalishaji wadogo hawakuweza kukidhi mahitaji ya kibeberu ya wakati huo, hivyo ilibidi wanyang'anywe ardhi ili Wazungu waingie.

Kati ya mwaka 1945 na 1955, masetla wa Kiingereza waliongezea maeneo waliyomiliki kutoka ekari 287,635 hadi ekari 1,301,654; wa Kigiriki walipanua maeneo yao kutoka ekari 90,803 hadi ekari 294, 649; na, Wahindi walipanua maeneo yao kutoka ekari 68,110 hadi ekari 235,715. Kampuni ya Chakula ya Uingereza (Overseas Food Corporation) ambayo ilianzisha Mradi wa Ulimaji Karanga ilikuwa na malengo kufungua mashamba yenye ekari million 3 huko Kongwa na Lindi. Ilianza kwa kutwaa eneo la ekari 480,000 (ingawa iliweza kusafisha eneo la ekari 50,000). Hadi kufikia miaka ya 1950 asilimia 40 ya eneo la nchi lililoweza kulimika (ambalo lilikuwa asilimia 5) lilikuwa mikononi mwa masetla na makampuni ya kizungu. Kulikuwa na mabepari wa mashambani wa Kihindi na wa Kiaarabu pia kwa kiasi fulani, na baadaye hapo hata wale wa Kiafrika kama ilivyokuwa huko Mbulu, Ismani na kwingineko (Bates 1957).

Kufikia miaka ya 1950, upinzani dhidi ya utawala wa kienyeji uligeuka kuwa upinzani wa utawala wa aina yoyote wa mseto, kwani wenyeji walihisi kwamba utawala kama huo ulilenga kuimarisha mbinu za uporaji wa ardhi. Haya mapambano dhidi ya utawala wa machifu, wafanyabiashara wa Kihindi na unyanga'anywaji wa ardhi, hatimaye yaliiwezesha shughuli za Tanganyika African Association (TAA) ambayo ilikuwa imeundwa na wasomi wa Kiafrika tangu mwaka 1929 na kuwa TANU mwaka 1954 kuenea nchi nzima na kubadilika kimalengo na kuwa na msimamo mkali. Mgogoro wa ardhi wa Meru (1951-53) na kuongezeka kwa wasi wasi wa kuporwa ardhi miongoni mwa Waafrika ndivyo vilivyoanzisha uhamasishaji wa Watanganyika kupata ari ya kupigania uhuru wa nchi. Na ni mgogoro huu ambao ulipelekea kuanzishwa kwa TANU. Chanzo cha mgogoro huu ulikuwa ni mpango wa Kikoloni wa kutaka kunyang'anya ardi sehemu za Engare Nanuki na Liguruki kwa ajili ya kuwapatia Wazungu wafungue maranchi ya ufugaji kuanzia mwaka 1948.

Mgogoro wa Meru uligeuka kuwa suala la kimataifa ukiongozwa na Umoja wa Wananchi wa Meru—The Meru (Freemen) Citizens' Union. Mwaka 1951, wakoloni waliingia huko Meru na kuswaga mifugo ya Wameru, wakavunja na kuchoma nyumba, maghala na mazizi ya wenyeji na kuwafukuza Wameru kama nyangalika. Wameru walikataa kuhama na wakagoma kupokea fidia. Katika mapambano hayo, watu wawili waliuawa na wengine 25 kufungwa (idadi ya waliojeruhiwa haijulikani). Wameru waliwasilisha malalamiko yao kwenye ofisi ya makoloni, London, kasha walikusanya michango kutoka sehemu mbali mbali za nchi na

kumpeleka Kirilo Japhet, ambaye alikuwa kiongozi wa umoja wa Wameru na katibu wa TAA, na Earle Seaton ambaye alikuwa mwansheria kutoka visiwa vya West Indies Umoja wa Mataifa. Kirilo Japhet alikuwa Mwafrika wa kwanza kuuhutubia umoja wa mataifa, naye alifanya hivyo mwaka 1952 (Japhet & Seaton 1967).

Mnamo mwaka 1953, baada ya Nyerere kutwaa uongozi wa TAA pamoja na Saadani Kandoro walimwomba Kirilo Japhet azungukie nchi nzima chini ya mwavuli wa TANU kuwaleza wananchi kuhusu mgogoro wa Meru. Hili lilisababisha mwamko mpya nchi nzima, kiasi kwamba liliwafanya Nyerere, Kirilo, Kandoro, John Rupia, watoto watatu wa Kleist Sykes, Dossa Aziz, na wengine kuanza kuibadilisha katiba ya TAA. Mapambano ya wakulima yalikuwa yamegeuka kuwa mapambano ya kitaifa dhidi ya ukoloni. Hata tume ua Umoja wa Mataifa iliyotembelea Tanganyika mwaka 1954 ilikiri wazi kwamba suala la ardhi kitovu cha maasi yote yaliyokuwa yakitokea nchini, na kwamba mgogoro wa Meru ulikuwa umesababisha wenyeji wa nchi nzima kuungana ili kuwapinga wale wote wasio wenyeji.

Kisiasa, hii migogoro ya ardhi miongoni mwa wana TANU ilibainishwa na ukosoaji wa sera za kikoloni za mfumo wa mseto kufikia mwaka 1956. Nyerere alidai wazi kwamba wale waliosimamia siasa hizo walikusudia kuzigeuza siasa za ubaguzi wa rangi ili ziwe za ubaguzi wa kifedha—ambazo zingekuwa mwendelezo wa siasa za kulinda watu wachache. Sera za mseto zilikusudia kutambua umilikaji binafsi wa ardhi na uwezekano wa kununua na kuuza ardhi bila kujali rangi, kwa kisingizio cha usawa. Nyerere alitamka wazi kwamba sera hizo zingepelekea ardhi yote kumilikiwa na wahamiaji ambao ndio walikuwa na fedha na ufadhili kutoka katika nchi walizotokea (Nyerere, kama hapo juu). Mwaka 1958, TANU ilizikataa sera za soko huria katika masuala ya umilikaji wa ardhi. Ilitamka wazi kwamba kile kilichokuwa kikifanywa na serikali ya kikoloni ni kubadilisha mfumo wa unyang'anyi wa ardhi ili kuwezesha kuwepo mfumo wa kuwakosesha wenyeji ardhi kwa njia ya umiliki ambao umejikita katika umiliki binafsi wa ardhi kutegemeana na uwezo wa mtu kimtaji, na hivyo kuwafanya wale walio katika hali ya chini washindwe kumiliki ardhi.

Kwa kifupi, msingi wa mapambano ya uhuru na mwamko wa kitaifa katika nchi yetu ilikuwa ni upiganiaji wa ardhi na raslimali zake. Wale wapendao kuipindisha historia kwa maslahi ya makundi yao na ya wakoloni hudai kwamba TANU ndiyo iliyoleta uhuru. Lakini ukweli ni kwamba ni mapambano ya wakulima na wafanyakazi na makundi mengine ya wanyonge yalyowalazimisha wakoloni kuipa Tanganyika uhuru. Wasomi walioanzisha TANU walilazimishwa kuchukua huo msimamo wa kitaifa/kizalendo na mapambano hayo. Na wasomi waliokubali kuongoza mapambano hayo ni wale tu waliokuwa na mioyo jasiri. Wale waliokuwa na mioyo fufutende walibakia hawana msimamo au waliendelea kujipendekeza na kujikomba kwa Wakoloni.

Uhuru, Maendeleo na Kuporomoka kwa Uzalendo

Upinzani huo wa kuporwa ardhi na raslimali wa wakati wa ukoloni ulikuja kuwa msingi wa sera za serikali huru. Kwa watawala wapya, kwao huu haukuwa upinzani dhidi ya umilikaji binafsi wa ardhi; bali dhidi ya umilikishaji wahamiaji ardhi. Kwa sababu hiyo, baada ya uhuru ilitamkwa rasmi kwamba ardhi ni mali ya taifa, na ni serikali tu iliyokuwa na uwezo wa kutwaa au kugawa ardhi kwa manufaa ya umma. Tamko hilo lilitolewa bila ya kuibadilisha sheria ya kikoloni ya umilikaji wa ardhi ya mwaka 1923. Hii sera iliendana zaidi na sera za watawala wapya kuliko kuainisha hali halisi kama ilivyokuwa. Msimamo wa viongozi wa mapambano ya uhuru ulikuwa umeanza kubadilika ghafla mwaka 1958 baada ya TANU kushinda katika uchaguzi wa mseto na kuwawezesha Waafrika kuingia katika Baraza la Kutunga Sheria (Legislative Council).

Kwa mfano, ingawa TANU ilikuwa imejijenga katika maeneo ya Ziwa Victoria kwa misingi ya kuwaunga mkono wakulima katika mapambano yao dhidi ya sera za kilimo zilizotishia mfumo wa maisha ya watu, wakulima wa huko waliamua kuzidisha mapambano yao dhidi kanuni zote zilizotolewa na serikali za machifu. TANU iliwaambia Wasukuma huko Mwanza kwamba ilibidi watii sheria na kudumisha utulivu, kwani kila serikali ina sheria zake. Wakaambiwa kwamba "TANU ya leo" iko tofauti kabisa na "TANU ya Jana" (Taylor 1963: 141). Hivyo ndivyo walivyoambiwa Waluguru, Wasambaa, Wahehe, na wenginewe ambao walikuwa wameamua kuzidisha ari ya mapambano dhidi ya sheria za kikoloni zilizohusu ardhi na matumizi yake. Hata wafanyakazi wa mkonge wa Tanga, wa migodini Mwadui na wa reli na posta ambao walizidisha mapambano yao nao waliambiwa hivyo hivyo na TANU (Friedland 1969). Lakini haya mapambano ya wafanyakazi ni historia nyingine ambayo inahitaji majadiliano yake ya kina na si katika mada hii.

Ukweli ni kwamba, kipindi kabla na baada ya uhuru kilikuwa ni kipindi cha mapambano na migongano mikubwa ambayo ilitokana na uelewa tofauti wa maana halisi ya kujitawala—kisiasa, kiuchumi na kijamii—miongoni mwa makundi na matabaka mbali mbali nchini. Kilikuwa kipindi ambacho watu walipigania kuzimudu wao wenyewe nyenendo za nyanja mbali mbali za kimaisha, kisiasa na kiuchumi kwa nia ya kuyabadilisha maisha yao. Mwandishi mashuhuri wa kizalendo, Sheikh Shabaan Robert aliyaainisha haya katika kitabu chake cha mwaka 1960 kwa kubainisha kwamba kulikuwa na misimamo miwili kuhusu uelewa wa mabadiliko yaliyokuwa yanatokea Tanganyika kutokana na kupewa nafasi ya kujitawala wenyewe: kuna baadhi ya watu ambao waliyatazama mabadiliko hayo kama matokeo ya mapambano dhidi ya ugawanywaji wa mali, faida na madaraka usio na usawa miongoni mwa watu nchini; na wengine waliona kuwa haya yalikuwa matokeo ya mabadiliko yasiyoepukika kutokana na ukweli kwamba yalikuwa yakitokea duniani kote (Robert 1966).

Mwaka 1957-58, Shabaan Robert alikuwa ameandika shairi refu—*Mapenzi Bora,* ambalo lilitetea mapenzi miongoni mwa binadamu (Robert 1969) na mwaka 1960-61 aliandika riwaya—*Siku ya Watenzi Wote*, ambayo ilijaa umaizi na utambuzi wa masuala ya maendeleo

na ustawi wa watu; matamanio ya watu na mahitajio ambayo yangewawezesha kuyabadili maisha yao yaliyokuwa yamepogoshwa na utawala wa kikoloni; kuhusu ukosefu wa imani katika dini na kanuni za maisha; harakati za wanawake kujitafutia usawa na fursa ya kushiriki katika maamuzi mbali mbali; uharibifu uliokuwa umetokea katika tabia za mwenendo wa maisha ya watu; na mengine mengi ya msingi. Katika riwaya hii, Shabaani Robert alionyesha jinsi watu walivyokuwa wakipigania ujenzi wa jumuia zenye uwiano kimantiki.

Wakulima walitegemea kwamba baada ya wakoloni kuondoka matumizi ya nguvu katika kuwalazimisha kulima mazao yaliyopangwa na serikali au kutekeleza sera za kilimo yangekwisha. Pia waliamini kwamba unyang'anyi wa ardhi ungekomeshwa. Kwao uhuru maana yake halisi ulimaanisha kujitawala wenyewe na kujiamulia mambo kuhusu maisha yao. Kwa mfano, mnamo Septemba 1959, kikundi cha vijana 90 wasiokuwa na kazi, wakulima, n.k. kiondoka mjini Morogoro kuelekea mahali kusikojulikana. Baada ya muda ilikuja fahamika kwamba walikuwa wamekwenda Kilombero kuanzisha mashamba ya kilimo cha umoja na walikuwa wameshasafisha mashamba ya ekari 45 baada ya wiki moja. Enzi za uanzishaji wa makazi ya pamoja na uzalishaji wa kushirikiana zilikuwa zimeanza, na kati ya mwaka 1960 na 1963 kulikuwa na maelfu ya miradi kama hiyo iliyokuwa imeanzishwa na wananchi kwa ridhaa yao wenyewe (Cliffe & Cunningham 1973; Wisner na wengine 1973; Coulson, kama juu).

Mfano wa makazi na uzalishaji wa aina hiyo uliosifika sana enzi hizo ni ule wa Ruvuma development Association, chama kilichounganisha vijiji 17. Hivi vilikuwa vijiji vilivyoendelea sana kijamii, kidemokrasia na kiuchumi. Ni vijiji vilivyoanzisha shule zake na mitaala yaliyozingatia mahitaji ya jumuia zake; vikaanzisha viwanda vijijini; na kujitosheleza kwa mahitaji yote. Vijiji vya RDA, na vingine ambavyo vilianzishwa na wananchi wenyewe sehemu mbali mbali vilipata mafanikio makubwa. Na wakati mwingine TANU na serikali ilijitokeza na kuvisifia huku ikiwapa baadhi ya misaada. Lakini sera za serikali mwanzoni mwa miaka ya 1960 zilikuwa zimelenga kuanzisha tabaka la mabepari wa kiafrika wa mashambani. Hizi sera zilianguka kitakotako na hazikufaulu hata kidogo. Na ni kwa sababu hii, serikali ilijikuta ikiwa na migogoro na vijiji vilivyoanzishwa na wananchi wenyewe, kwani havikutaka kudhibitiwa. Vijiji vya RDA vilivunjwa na serikali na mali zao zote kunyang'anywa mwaka 1969, baada ya wanavijiji hao kukataa kulima tumbaku wakisisitiza kwamba kwao chakula cha mazao ya chakula yalikuwa muhimu zaidi.

Watu wa makondeni walikuwa wamekusudia kwa dhati kuyakana mahusiano yaliyoletwa na wakoloni pamoja na mfumo wa maisha ulioyaleta. Hapa nitatoa mfano tofauti kidogo wa mapambano yaliyolelekezwa katika masuala ya mfumo wa maisha mara tu baada ya uhuru—wa Wambugwe waliokuwa wakiishi Kusini mwa Ziwa Manyara. Wambugwe waliamini kwamba uhuru ulimaanisha watu wajitawale wenyewe na wawe na uwezo wa kufanya maamuzi yanayohusu maisha yao. Kutokana na njaa na matatizo yaliyotokea mara tu baada ya uhuru, wazee walilalamika kwamba maisha yalikuwa hayajabadilika, ingawa walikuwa

wamepata uhuru. Wakajiuliza iweje kwamba hawakuruhusiwa kuwa na waganga wa mvua (msungati) katika kila wilaya, badala ya hawa machifu ambao walikuwa wamechomekewa na wakoloni hata baada ya uhuru? Wakadadisi zaidi: iwapo wako huru, iweje basi walikuwa wanendelea kulipa kodi? Na, kwa nini hawaruhusiwi kuwinda wanyama bila kulazimika kutafuta leseni? (Mbee 1970: 138).

Ingawa vijana wa TANU walijaribu kufafanua kwamba maana ya uhuru haikuwa hiyo, wazee walishikilia msimamo wao kwamba hawakubaliani na vitu ambavyo haviko tofauti na wakati wa utawala wa Waingereza. Mwaka 1963, wazee hao waliitisha mkutano mkubwa ambao ulijadili kuhusu suala la kurudia mfumo wao wa asili wa kulinda mashamba yao. Wakatamka wazi kwamba, sababu yao kuu ya kufurahia uhuru ni kurusishia mila zao. Tamka lao la kwanza lilikuwa: waganga wa kienyeji sharti waheshimiwe, na hasa wale wa miti shamba na wale ambao wanalinda kaya za watu na jumuia dhidi ya maradhi. Walidai kwamba kwa sababu walikuwa huru walikuwa na haki ya kuhakikisha kwamba nchi yao inatakaswa ili iweze kuzalisha chakula kingi. Kwa maelezo yao, juhudi zao za kuweza kufanya hivyo zilikuwa zinakinzwa na Wakatoliki na kanuni za kikoloni zilizoendelezwa na serikali ya baada ya uhuru (Mbee: taz. juu).

Ukweli ni kwamba japokuwa nchi ilikuwa huru, uhuru huo ulikuwa ni wa bendera na nchi iliendelea kuwa tegemezi. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu (1961-64) ulikuwa umeandaliwa na Benki ya Dunia. Mpango huu uliitaka serikali ya Tanganyika itafute kila njia ya kuwezesha kuwe na mazingira mazuri ambayo yangewavutia wawekezaji wa nje kuwekeza katika sekta za viwanda, madini, kilimo, huduma, kodi na ushuru nafuu au hata msamaha kwa wawekezaji, kuwapa mikopo, na hata ruzuku kwa ajili ya wawekezaji, n.k. Ilibidi nchi ijenge mazingira mabayo yangewezesha kuwepo kwa mfumo wa ujira ambao ni wa chini, bei za mali ghafi ambazo ni nafuu na fursa ya wawekezaji kuhamisha faida zao na kuzipeleka nje. Mpango huu ulipendekeza kwamba kuundwe shirika la umma la maendeleo ambalo lingesaidia kuvutia mitaji ya ziada na hata kuwezesha serikali kuingia katika ubia na wawekezaji wa nje (Chachage 1986).

Haya yote yalitegemea uwezo wa nchi kuongeza uzalishaji wa bidhaa za kuuza nchi za nje. Hivyo kilimo kilikuwa ndiyo msingi wa maendeleo. Kutokana na mwelekeo huo, matumizi ya nguvu katika kuwalazimisha watu walime kahawa, tumbaku, chai na mazao mengine yaliongezeka. Kadhalika, migomo ya wafanyakazi iliharamishwa. Katika mikoa na wilaya mbali mbali kulikutungwa sheria ndogo ndogo za kuwalazimisha watu watu wabadilishe mfumo wa ukulima na kuzalisha mazao ya kuuza nje ya nchi. Haya yalitokea, kwa mfano, Kigoma, ambako wakulima walilazimishwa kulima pamba; Ruvuma ambako wakulima walipangiwa ukubwa wa eneo la kulima tumbaku; n.k. Kuliwekwa pia adhabu za kifungo na faini kwa watu waliokiuka sheria hizo. (Coulson 1982: 266; McHenry, Jr 1973: 303-316).

Kufutwa kwa utawala wa machifu mwaka 1963 kuwezekana kwa sababu kwa wananchi wengi, wao waliwakilisha maslahi ya wakoloni. Hivyo hakukuwa na upinzania kabisa. Lakini badala yake kulikuwepo uimarishaji wa serikali za wilaya na nguvu za maafisa wa serikali, watendaji na hata majumbe. Mwaka huo huo, serikali ilipitisha sheria ya uwekezaji ambayo ilizingatia ushari uliokuwa umetolewa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu. Kwa kifupi, mikakati ya maendeleo ya nchi iliyotekelezwa katika miaka kumi ya mwanzo ya uhuru ilisisitiza haja ya serikali kusimamia kila shughuli—za maendeleo, ujenzi wa barabara, uanzishaji wa vyama vya ushirika na bodi za kununua mazao, utoaji ruzuku kwa wakulima, utoaji huduma za afya na elimu na huduma nyingine. Mikakati hiiilimaanisha uimarishaji wa serikali kuu, udhoofishaji wa jumuia zote zisizokuwa za kiserikali ambazo zilizojishughulisha na utoaji wa huduma wakati wa ukoloni, kutokana na serikali kutokutoa huduma kama hizo na ufishaji kwa ujumla upinzani kutoka kwa wafanyakazi, wakulima na makundi mengine ikiwa ni pamoja na ule wa kisiasa.

Lengo, kama walivyobainisha watawala wa baada ya uhuru, lilikuwa ni kuleta maendeleo na ustawi wananchi kwa ujumla. Hivyo dola ya utawala wa kikoloni ilianza kuchukua sura mpya: ile ya kusimamia na kupanga mipango ya maendeleo. Na ili kuyafikia maendeleo hayo, ilibidi uhuru wa vyombo vya kulinda na kutetea maslahi ya wananchi, kama vile vyama vya wafanyakazi, wakulima, vijana, n.k. vipunguziwe nguvu zake au viwekwe chini ya udhibiti wa serikali. Wakulima hawakutakiwa wadai bei nzuri ya mazao yao au hali bora ya uzalishaji, kwani hili lingepunguza uwezekano wa serikali kukusanya mitaji ya kuwezesha kuleta maendeleo na wafanyakazi hawakutakiwa kudai ujira mnono kwa kuwa hilo lingewatishia wawekezaji. Ukweli ni kwamba mkakati huu uliwezesha ukuaji wa uchumi katika miaka ya 1960, ingawa masetla walikuwa wametoroka nchi pamoja na mitaji yao na hakukuwa na wawekezaji wengi kutoka nje kama ilivyotarajiwa.

Katika sekta ya kilimo, iankadiriwa kuwa kulikuwa na ekari milioni 29 ambazo zilikuwa zikilimwa mwaka 1964. Eneo hili liliongezeka na kufikia ekari milioni 39 mwaka 1970. Katika kipindi hiki, uzalishaji wa pamba ulipanda kutoka tani 30,000 hadi tani 79,000; kahawa kutoka tani 20,000 hadi tani 55,000; pareto kutoka tani 1,300 hadi tani 3,800; sukari kutoka tani 29,000 hadi tani 90,000; korosho kutoka tani 28,000 hadi tani 118,000; na, alizeti kutoka tani 6,000 hadi tani 13,000. Ni haya maendeleo katika sekta ya kilimo amabayo yalwezesha ukuaji wa uchumi wan chi kwa ujumla. Hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya 1960 viwanda vingi vilikuwa vimejengwa, kiasi kwamba mahitaji yote ya kawaida ya nchini yalikidhiwa na viwanda hivyo. Kutokana na hili, serikali ilikuwa imeanzisha mpango wa miaka 20 wa ujenzi wa viwanda vikubwa (heavy industries) mwaka 1971. Kulikuwa na mashirika 64 ya umma mwaka 1967 na idadi yake ilipanda hadi 139 mwaka 1974, na kufikia 320 mwaka 1982. Haya mashirika yalikuwa na viwanda au makampuni tanzu kadhaa chini yake. Kwa mfano, Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) lilikuwa na zaidi ya viwanda 3,200 vilivyokuwa vimetapakaa katika miji yote nchini.

Katika masuala miundo mbinu, kutoka kuwepo kwa kilomita 200 tu za barabara za lami, na barabara nyingi zilizokuwa zikipitika kwa msimu, kufikia miaka ya 1970 kulikuwa na barabara za lami kutoka Dar es Salaam hadi Namanga, Dar es Salaam hadi Zambia, Dar es salaam hadi Rufiji na Morogoro hadi Dodoma. Hata zile barabara ambazo hazikuwa na lami zilikuwa zimeboreshwa. Kadhalika Tanzania (pamoja na Zambia) ilikuwa ni nchi pekee iliyokuwa imejenga reli—Tanzania Zambia Railway (TAZARA)—katika bara zima la Afrika baada ya uhuru. Kulitokea maendeleo makubwa pia katika sekta ya afya kutokana na kujenga vyuo mbali mbali na vya ngazi tofauti za mafunzo ya wauguzi na madaktari. Kati ya madakatari waliosajiliwa 403 mwaka 1961, Waafrika walikuwa 12 tu na wale wenye leseni walikuwa 22 tu. Idadi ya madaktari wa Kiafrika ilifikia 123 mwaka 1970, na idadi ya hospitali ilikuwa imefikia 122 mwaka 1971 ikilinganishwa na mwaka 1961 wakati kulipokuwepo hospitali 98; idadi ya vituo vya afya vijijini ilipanda katika kipindi hicho hicho kutoka 22 hadi 90; na idadi ya zahanati za vijijini ilipanda kutoka 975 hadi 1,400. Wakati kulikuwa na miradi 20 tu ya maji mwaka 1961 na watu 300,000 walikuwa na huduma za maji safi vijijini, kufikia mwaka 1971 kulikuwa na miradi ya maji zaidi ya 100 na watu 1,400,000 walikuwa na huduma za maji safi (Nyerere 1973).

Katika nyanja ya elimu kulikuwa na hatua kubwa imepigwa pia, kwani wakati kulikuwa na watoto 486,000 waliokuwa katika shule za msingi 3,100 mwaka 1961, hadi kufikia mwaka; kulikuwepo watoto 848,000 (asilimia 54 ya watoto wote waliostahili kuwa shuleni) katika shule za msingi 4, 705. Lengo la watoto wote wenye umri wa kwenda shule kusomeshwa lilifikiwa mwaka 1975. Kadhalika, wakati kulikuwa na wanafunzi 11,832 katika shule za sekondari (176 wakiwa kidato cha tano na sita) mwaka 1961, idadi yao ilifikia 31,662 mwaka 1971 na kati yao, 1,488 walikuwa katika kidato cha tano na sita. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilijengwa baada ya uhuru na kilishakuwa na wanfunzi 3,000 mwaka 1971. Ikumbukwe pia kwamba Watanzania kwa ujumla walikuwa hawajui kusoma na kuandika wakati nchi ikipata uhuru, lakini kutokana na kampeini za elimu ya watu wazima, mwaka 1971, watu wazima 560,000 walikuwa wakihudhuria masomo ya watu wazima na idadi ya wale waliokuwa wamejiandikisha katika masomo hayo ilipanda hadi milioni 5 mwaka 1977. Asilimia 95 ya Watanzania walikuwa wanjua kusoma na kuandika ilipofika mwaka 1982.

Japokuwa sera za baada ya uhuru zikiwa ni pamoja na zile za ardhi zililenga kuinua maisha ya watu wa kawaida na kuwalinda wazalishaji wenyeji, kihalisia zilikuwa na madhara yake pia, kwani hizi ndizo zilizowezesha serikali baada ya uhuru kupora maeneo mengi ya wafugaji na wawindaji kwa kisingizio cha maendeleo. Kadhalika, ni sera hizo zilizoiwezesha serikali kuwahamisha watu wa mashambani kwa nguvu mwaka 1973/74 (Operesheni Vijiji) kutoka katika maeneo yao na kuwakusanya vijijini. Kwani misingi ya sera hizi ilikuwa imejikita katika mahusiano yaliyoanzishwa na ukoloni. Idadi ya mbuga za wanyama ilifikia 12 hadi mwaka 1995. Wakati huo huo, kulikuwa na maeneo 17 ya hifadhi za wanyama na maeneo 40

yaliyokuwa chini ya udhibiti wa serikali. Kwa kifupi, kilomita za mraba 239,065 au asilimia 26 ya eneo la nchi (kilomita za mraba 945,166) zilikuwa chini ya himaya ya serikali. Kadhalika ni sera na sheria hizo zilizowezesha serikali kutwaa maeneo makubwa ya ardhi kwa ajili ya mashamba ya taifa, ikiwa ni pamoja na kuwapokonya wenyeji wa Mbulu, kwa mfano, maeneo yao kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha ngano.

Mafanikio haya katika masuala ya maendeleo yaliambatana na migogoro yake. Kufikia mwaka 1965, kwa mfano ilibainika kwamba vyama vya ushirika ambavyo vilikuwa vimeanzishwa an serikali vilikuwa vikiwanyonya na kuwaibia wakulima. Kadhalika vilikuwa vimejaa ufisadi na viliwafaidia watu wachache waliokuwa madarakani. Wakulima walionyesha wazi kukerwa na mambo kama hayo pamoja na ulipishwaji mkubwa wa kodi. Kilichowakera zaidi ni jinsi ambavyo wale waliokuwa katika madaraka ambao walikuwa wamekabidhiwa dhamana ya kuwatumikia wananchi walivyokuwa wakijineemesha, hadi ikafikia wakati wakaitwa kwamba wao ni kabila la *Wabenzi*. Waliitwa hivyo baada ya Waziri wa Tawala za Mikoa kupuuzia amri ya Rais na kuagiza Mercedes Benz 17 kwa ajili ya wakuu wa mikoa. Wabenzi wakawa wanaitwa wanyonyaji na makupe *wa makabwela* (Coulson 1982: 182; Karioki 1979: 86). Enzi hizo Wasukuma waliimba wimbo uliosema (Maguire: 1967: 369):

> Sisi Watanzania tunajitawala wenyewe
> Lakini kuna wachache wanaofaidi matunda ya watu waliopata uhuru.
> Hawa wana madaraka makubwa serikalini
> Wanapata mishahara minono,
> Lakini sisi wakulima hatutafaidika
> Utumwa bado ungalipo.
> Majira ya mvua yanakaribia
> Na sisi tunalima pamba:
> Tutakachoona ni bei ya pamba kuteremka.
>
> Waungwana, tunawatajirisha watu wengine,
> Tunawafanya wanenepe na kuneemeka.
> Ebu angalia saa zao mikono walizovaa
> Na jinsi wanavyovitunia vitambaa vyao kufuta pua zao!

Hadi hapa, haistaajabishi kwa nini Azimio la Arusha lilitangazwa mwaka 1967. Azimio hili lilitangaza vita dhidi ya wanyonyaji wa nje na ndani na kutangaza azma ya nia ya ukombozi. Kama kumewahi kutokea maandamano na matendo mengine makubwa nchini ya kuunga mkono sera, hakuna kama ilivyokuwa mwaka 1967!

Lakini Azimio hili halikuweza kuzuia vitendo vya kidhalimu vya wanyonyaji na wale waliowakandamiza wananchi. Matendo ya kuwashurutisha wananchi yaliendelea na kadhalika unyonyaji wa wakulima uliendelea. Badala ya kuwapa wananchi uhuru zaidi, hatima ya sera hizi ilikuwa ni kuwadhibiti wakulima na shughuli zao kuliko hata ilivyokuwa awali. Ni katika

hali hii ndipo nchi iliposhuhudia watu wakiswagwa kama mifugo na kukusanywa katika vijiji vya maendeleo/ujamaa, wakilazimika kuacha ardhi na mazao yao porini. Kati ya mwaka 1973 na 1975 kiasi cha karibia watu million 9 wa makondeni walihamishwa na kuwekwa vjijini, na mwaka 1976 ilitangazwa rasmi kwamba nchi nzima huko mashambani watu walikuwa wakiishi katika "vijiji vya maendeleo". Kutoka idadi ya vijiji 809 nchini mwaka 1969, idadi ya vijiji ilikuwa imeongezeka hadi I,950 mwaka 1970. Hadi kufukia mwaka 1973, kulikuwa na vijiji 5,628 na mnamo mwaka 1976 idadi ya vijiji hivi ilifikia 7,684 (Mapolu 1986: 118-9)

Kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni, serikali ilitumia mabavu kuwahamisha watu wa makondeni. Si hivyo tu: watu wengi walihamishwa kutoka kwenye maeneo yenye neema na kupelekwa kwenye maeneo ambayo yalikuwa hafifu kwa shughuli za kilimo au yale ambayo yalikuwa na uhaba wa ardhi. Kadhalika, kuna baadhi ya wananchi walihamishwa wakati wa majira ya kilimo—wakati mvua zikinyesha. Makazi ya zamani ya wananchi yaliharibiwa pamoja na mali zao. Watu waliwajibika kupoteza muda wao mwingi kujenga makazi mapya, badala ya kujishughulisha na masuala ya kilimo. Kadhalika, sehemu kubwa za misitu ambazo watu walikuwa wamezoea kuzihifadhi kimila kama vyanzo vya kuni, miti ya majengo, matunda, dawa, na matumizi mengine, ziliteketezwa kutokana na mahitaji yaliyoibuka ghafla ya miti ya majengo na haja ya kufungua mashamba mapya.

Toka wakati huo, matatizo lukuki ya kimazingira na kijamii yaliibuka huko makondeni kutokana na kuchipuka ghafla kwa "vimiji" vidogo. Kadhalika, uzalishaji wa mazao uliporomoka ghafla, kiasi kwamba thamani ya bidhaa zilizokuwa zikiuzwa nchi za nje iliteremka kwa asilimia 35 kati ya mwaka 1974 na 1980. Mchango wa kilimo katika pato la taifa ulianguka kutoka asilimia 42 hadi asilimia 36 na wa viwanda uliteremka kutoka asilimia 11 hadi asilimia 4 kati ya mwaka 1975 na 1980. Kuporomoka kwa mchango wa viwanda kulitokana na kuadimika kwa mali ghafi kutoka nje ambazo zilinunuliwa na fedha za kigeni zilizotokana na uuzaji wa mazao ya kilimo katika soko la dunia. Kutokan na hali hiyo kwa ujumla, deni la taifa la nje lilikuwa limefikia shilingi bilioni 6 mwaka 1980. Si hivyo tu: kwa kuwa viwanda vingi vilikuwa vinazalisha chini ya uwezo wake—vingi vikizalisha wastani wa ya asilimia 35 wa uwezo wake—nchi ilikumbwa na uhaba mkubwa wa bidhaa zote muhimu, ikiwa ni pamoja na sukari, nguo, madawa, pembejeo, n.k.

Kibaya kuliko vyote hadi kufikia kipindi hicho ni ukweli kwamba mabodi ya mazao ambayo yalikuwa vyombo vya serikali vya kununua, kuuza na kuhudumia mazao mbali mbali, na kuiwezesha serikali kupata mapato kutoka kwa wakulima kwa ajili ya kujiendeleza na kupanga mipango ya maendeleo, yalikuwa yamegeuka kuwa mapango ya hasara. Haya yalikuwa yamejaa ufisidadi, wizi, ubadhilifu na ufujaji wa kila aina kuanzia miaka ya 1975, hususan baada ya vyama vya ushirika kufutwa mwaka huo baada ya kuzifuta serikali za mitaa kwa kisingizio cha kupeleka madaraka mikoani mwaka 1972. Toka mwaka 1975, zilikuwa zimeundwa serikali za vijiji ambazo pia zilikuwa na jukumu la kuwa vyama vya msingi kama

mawakala wa mabodi na mamlaka ya mazao. Kila kijiji kikawa na mameneja/watendaji wa serikali. Nchi ilishuhudia mabodi yakiwakopa wakulima pasi kuwalipa au kuwacheleweshea malipo yao, na pindi wakulima walipolipwa, mapato yalikuwa duni sana kulinganisha na thamani ya jasho lao.

Huu mpango wa kuwalazinisha wakulima kuishi katika vijiji ulikuwa umewachukiza sana watu wa makondoni tangu ulipoanzishwa. Katika baadhi ya sehemu, wakulima waliipinga serikali na chama wazi wazi. Huko Njombe, kwa mfano, wakulima walimwuua Bwana Shamba ambaye alikuwa akizitekeleza sera hizo. Kesi yao ilimalizika mwaka 1979. Mahakama iliwaachia kwa sababu sheria ilikuwa hairuhu kuharibu mali ya mtu na kila mtu alikuwa na haki ya kulinda mali yake. Walipolazimishwa kuanzisha mashamba ya kijiji, walifanya hivyo kwa shingo upande, kwa kuhisi kwamba walikuwa wakigeuzwa kuwa watumwa wa serikali. Hivyo, walitumia masaa siyo zaidi ya sita kwa wiki katika shamba la kijiji, wakifanya kazi kimgomo baridi. Walipoona mabodi nayo yamezidi kuwakopa, walianza kung'oa kahawa na kupanda nyanya na vitunguu (kama ilivyotokea huko Kilimanjaro) au waliicha miskorosho porini na badala yake kujishughulisha na kazi ya kuchoma mkaa ambayo ilikuwa na faida zaidi kwa watu wengi wa mkoa wa pwani. Kadhalika, wengi wao walianza kuyakwepa masoko ya serikali na kuuza mazao yao kwa walanguzi, ambao waliyapeleka nje ya nchi.

Operesheni vijiji lilisababisha matatizo mengi sana ya umilikaji wa ardhi. Kutoka wakati huo, watu waliweza kunyang'anwa ardhi ambayo iligawiwa kwa watu binafsi kutoka nje ya kijiji na hata taasisi ana serikali yenyewe. Hivyo ndivyo serikali ilivyoweza kutwaa maeneo makubwa ya ardhi hata za vijiji kwa ajili ya kufungua mashamba ya serikali. Leo hii maeneo hayo, badala ya kurushwa kwa wakulima, yanagawiwa/yanauziwa wawekezaji. Kufikia mwanzoni mwa miaka ya 1980, tayari kulikuwa na migogoro na kesi nyingi za ardhi. Hadi kufikia miaka hiyo hiyo, tayari kulikuwa na watu ambao walikuwa hawana ardhi katika baadhi ya sehemu za nje—kama hali ya mkoa wa Arusha inavyohihirisha hadi leo. Katika miaka ya 1980 nchi ilianza kushuhudia wimbi jipya la uvamizi wa ardhi, mali asili ana madini uliofanywa na watu wa mijini, na hasa maofisa wa serikali na wale wenye uwezo kifedha pamoja na mashirika ya kigeni. Serikali za vijiji zilikuwa zikigawa ardhi za vijiji kwa wageni na watu ambao ni matajiri ambao walishaonana dalili za uwezekano wa sera za ardhi kubadilika na kuwawezesha watu kumilikshwa. Ripoti ya Shivji imebainisha wazi hii migogoro iliyoanza miaka 1980s (Tanzania, United republic of 1994). Ingawa sera ya nchi ilisimamia kuwa ardhi ni mali ya taifa, biashara ya kununua na kuuza ardhi pamoja na kuwapora wakulima wadogo ilikuwa imeshashamiri hadi kufikia kipindi hiki.

Mwanzoni, wimbi hilo lilitiwa msukumo na sera mpya za kilimo zilizotangazwa zilitangazwa mwaka 1982 ambazo zilipendekeza mfumo wa uzalishaji binafsi na uwezekano wa watu kumilikishwa ardhi (Tanzania, United Republic of 1982), na urudishwaji wa serikali za mitaa mwaka huo huo na vyama vya ushirika mwaka 1984. Hizi sera zilianzishwa kama njia ya kutatua matatizo yaliyokuwa yakiikabili sekta ya kilimo na kukuza uzalishaji. Lakini pia hizi

sera zilianzishwa wakati ambapo Tanzania ilikuwa imeanzisha mipango ya kurekebisha uchumi, ambayo kasi yake iliongezeka kuanzia mwaka 1986. Katika miaka hiyo, kuliwa na wazee wengi waliokuwa wakistaafu na watu waliostaafishwa na serikari kwa nguvu (siku hizi wanasema wamepunguzwa baada ya kufukuzwa kazi!), ambao kimbilio lao lilikuwa ni kutafuta maeneo ya ardhi hata kama yalikuwa yabakie kama amana kwa ajili ya matumizi ya baadaye au kuja kuyauza tena. Kadhalika, kulikuwa na wawekezaji wa ndani na nchi ambao walikuwa wakihimizwa kuwekeza katika sekta ya kilimo.

Tanzania ilikuwa imeingia katika kipindi kingine cha unyang'anyi na uporaji wa ardhi kutokana na kutekeleza masharti ya Benki ya Dunia na ya Shirika la Fedha la Dunia. Kutokana na hali hii kumekuwa na mapambambano ya hapa na pale ya wakulima wadogo, wafugaji na makundi mengine ambayo yamekuwa yakibetuliwa pembezoni na mfumo huu uliodumu miaka ishirini. Haya matatizo na migogoro ya ardhi, kwa mfano, yalisababisha vita kati ya wakulima na wafugaji mnamo mwaka 2000 huko Kilosa, Morogoro. Chanzo cha migogoro hiyo kikiwa ni uingiaji wa watu wenye uwezo kimadaka au kimali kutoka mijini na kutwaa maeneo ya ardhi. Mwaka huo, watu 30 waliuawa, wengi waliumia na wengine kama 400 hivi waliyakimbia maeneo hayo kukwepa shari ya vita. Jumla ya nyumba 77 za wakulima na wafugaji zilitiwa kiberiti (*Daily News* 20.12.2000). Na katika miaka hii ya karibuni kumekuwa na ripoti nyingi za aina hiyo katika vyombo vya habari.

Licha ya migogoro miongoni mwa wenyeji, watu wa vijijini wamejikuta mara kwa mara wakigombana na serikali. Hii miaka ya karibuni, kwa mfano, imeshuhudia wananchi wa Rukwa, Arumeru, Handeni, n.k. wakigomea kulipa kodi. Inasemekana kwamba, Wamaasai wa Saunye, huko Handeni walitangaza mnamo mwaka 2002 kwamba hawatalipa kodi ya mifugo hadi hapo watakapo dhihirishiwa kuwa kodi zao zimekuwa zinatumikaje miaka yote hii. Walisema kwamba walikuwa wanagoma kulipa kodi kwa sababu walikuwa hawapati huduma zozote kutoka serikalini. Walionya kwamba mtu yeyote yule ambaye angewafuata kukusanya kodi wangemshughulikia vilivyo (*Business Times* 15-21.11.2002). Katika tukio jingine, Mwanamke wa Kimaasai—Harriet Lemoriet—ambaye alikuwa akiwakilisha mtandao wa taasisi za jumuia yake isiyo ya kiserikali aliyekuwa akihudhuria mkutano wa Consultative Group (kati ya wafadhili na taasisi za fedha za dunia na serikali ya Tanzania) uliofanyika Dar es Salaam, aligoma kuongea kwa Kiswahili au kwa Kingereza. Alidai kwamba apatiwe mkalimani, kwa sababu alikusudia kuongea Kimaasai, watake wasitake.

Aliwaeleza wajumbe wa mkutano huo kwamba, "Katika uelewa wangu mkutano huu unatakiwa kujadili matatizo yawakabiliyo wakulima na wafugaji, wengi wao wakiwa ni watu wa makondeni, lakini tutaelewaje kama kinaendelea nini wakatihatuielewi hata lugha inayotumika katika kujadili masuala hayo?" (*The Guardian* 04.12.2002) Kufuatana na uelewa wake, mkutano huo ulikuwa umelenga kuwashirikisha watu katika kutatua tatizo la umasikini, lakini haikuyumkinika kama vipi watu washiriki katika lugha ya kigeni. Hii haikuwa haki kabisa

kwa umma wa Watanzania ambao wengi wao ni mafukara na wanaishi vijijini. Hawa wamekuwa wakisikia kuhusu masuala ya utawala bora na mbinu za ushirikishwaji katika kutatua matatizo; lakini wote hawakuwemo kwenye mkutano huo. Alitaka mikutano kama hiyo ikafanyike vijijini na siyo kwenye mahoteli makubwa ya mijini. Alihitimisha kwa kulaumu sera za serikali za kilimo. Kwa mawazo yake, hakukuwa na sababu ya serikali kuingiza chakula kutoka nchi za nje wakati wakulima walikuwa wakizalisha chakula cha kutosha na kingi kilikuwa kinaoza kutokana na ukosefu wa masoko ya uhakika. Waziri wa Fedha, Bwana Basil Mramba, alimjibu kuwa siku za nyuma, mikutano kama hiyo ilikuwa ikifanyikia Paris, kwa hiyo ni maendeleo makubwa kuwa sasa inafanyikia Dar es Salaam!! (*The Guardian* 04.12.2002)

Hitimisho

Napenda kutamka wazi kwamba misingi ya utaifa na uzalendo, hadi kufikia watu kuitwa wananchi, ni uwezo wao wa kumiliki na kudhibiti njia za kuzalisha mali na kujikimu kama watu binafsi, jumuia na hata taifa. Na katika hili mhimili mkuu ni umiliki wa ardhi na vilivyomo ndani yake. Uwezo huo ukififishwa basi watu wanaishia kuwa watawaliwa na watu wa nje, kitendo ambacho ni cha aibu sana katika karne hii ya 21, ambayo imehinikizwa na mahubiri ya demokrasia, kushirikishwa, uwezo wa watu kujiamulia mabo yao wenyewe, haki za binadamu, n.k. Inavyoelekea, maneno ya mwanamapinduzi Frantz Fanon (2001) aliyotamka wakati nchi za kiafrika zikipata uhuru yamesadifu: watu wa mijini na hususani mabwanyenye wa kitaifa mara nyingi huishia kuhaini mapambano ya kitaifa. Baada ya uhuru matamanio yao ni kupata makombo ya mabwana waliokuwa wakitutawala na wanaendelea kututawala. Hawawezi kufikiria kwa kuzingatia maslahi ya taifa na matatizo yake, na wanaridhika kuwa mameneja na watekelezaji wa maslahi ya nchi za magharibi na mashirika yake.

Kama tukizingatia mkutadha wa mapambano ya sasa hivi ya wazalishaji wadogo, basi ni wazi kwamba uamsho wa hisia za kizalendo umeanzia tena miongoni mwa watu wa vijijini. Kilichokosekana ni wasomi wa umma ambao wako tayari kuungana nao katika vuguvugu hili, kwani badala yake kuna asasi zisizo za kiserikali ambazo zimejipandikiza kwa kisingizio cha kuwatetea huku zikijinufaisha na kuendelea kuwepo kwa mfumo unaowafukarisha wananchi.Na hapa yanibidi niseme wazi kwamba dhana ya utandawazi iliyojikita katika vichwa vya watu wengi, hasa wasomi na wanasiasa wetu, ni dhana ya uzushi mtupu! Huu si utandawazi; bali ni utandawizi!

Inabidi kuyatilia mashaka haya madai kwamba kuna kipya katika hii dhana ya utandawazi. Kwa mfano, dai kwamba teknolojia imeufanya ulimwengu kuwa kijiji kwa kuwezesha watu wote duniani kuunganishwa kirahisi kwa mawasilino, limeibusha mjadala kuhusu suala uwezekano au fursa ya kuwa na vyombo vya masiliano kwa watu wote na hususan wale ambao ni mafukara au makabwela. Hakuna usawa katika hili, walio wengi duniani hawana fursa au nafasi ya kuwa washiriki wa hayo mawasiliano. Wenye fursa ni matajiri na wale wenye uwezo tu. Kadhalika, imedhihirika wazi kwamba maudhui ya

yaliyomo katika mawasiliano hayo ni yale ya upande mmoja—wa nchi za magharibi. Hivyo, kuna watoa habari na wapokea habari; watoa maarifa na wapokea maarifa; wenye uhodhi wa ukweli na wale ambao sauti zao hazisikiki kabisa, wastaarabu na washenzi, wenye utamaduni na wasio na utamaduni, lugha za manufaa na zile ambazo si muhimu, n.k.. Vyote vilivyo 'vyema' ni vya kutoka magharibi na vile visivyofaa, ni vile ambavyo ni vya kwetu wenyewe!

Kabla hii dhana ya utandawazi haijaanza kutumika, huu mfumo ulijilikana kama ni mfumo wa dunia wa mahusiano ya kibepari, ambao ulikuwa umeiunganisha dunia nzima kutokana na mapinduzi ya kimawasiliano na teknolojia. Hivyo ndivyo alivyoutambulisha mfumo huu Mwalimu J.K. Nyerere mwaka 1970 katika hotuba iliyonukuliwa hapo awali. Lakini kwake, badala ya mfumo huu kuleta ukombozi wa mwanadamu, ulikuwa ukiyakomaza mahusiano ya kinyonyaji; badala ya kuibuka kwa dunia moja matokeo yake yalikuwa ni mgawanyiko maradufu wa watu kitaifa na kimataifa kati ya mafukara (ambao ni wengi) na matajiri (ambao ni wachache). Kwa maneno yake mwenyewe:

> Kwa lugha ya utaalamu, dunia sasa ni kitu kimoja.[4] Binadamu ameitazama dunia kutoka mwezini akaona jinsi ilivyo kitu kimoja. Ninaweza kusafiri toka Tanzania hadi New York kwa saa chache tu kwa ndege za jeti. Mawimbi ya redio yanatuwezesha kuzungumza na wenzetu, ama kwa wema au kwa ubaya, mnamo kipindi cha sekunde baina ya mtu kusema na kusikiwa. Bidhaa hutengenezwa kwa vifaa vya ustadi kutoka sehemu zote za dunia, na halafu huuzwa maelfu ya maili kutoka mahali zinakotengenezwa.
>
> Lakini wakat huo huo ambapo, kwa sababu ya maendeleo ya ufundi [teknolojia—C.S.L.), kutegemeana kwa binadamu kunazidi, bado tabaka baina ya watu nazo zinazidi kupanuka kwa haraka zaidi siku hata siku…..
>
> Kwa hiyo dunia siyo kitu kimoja. Watu wake wamegawanyika zaidi sasa, na pia wanatambua zaidi migawanyiko yao, kuliko walivyokuwa hapo zamani. Wamegawanyika baina ya walioshiba na walio na njaa; wamegawanyika baina ya walio na mamlaka na wanyonge; wamegawanyika baina ya mabwana wanaotawala na watwana wanaotawaliwa; baina ya wanaonyonya na wanaonyonywa. Na watu wachache ndio wanakula vizuri, na ndio wanaomiliki mali ya dunia nzima na wanomiliki pia binadamu wenzi wao. Aidha, kwa ujumla, watu wachache hao ni weupe….(Nyerere 1974: 96-7)

[4] Hii makala ilitafsiriwa toka lugha ya Kiingereza mwaka 1974. Inaelekea kwamba neno teknolojia lilikuwa halitumiki wakati huo, kwani sentensi hii katika lugha ya awali inasomeka: "The world is one in technological terms". Tafsiri yake ilibidi iwe, "Kiteknolojia, dunia sasa ni kitu kimoja."

Kwa maoni yake yeye, katika dunia kama hiyo, hakuna masoko huria kati ya "mbilikimo" na "pandikizi la jambazi": bei ambazo ziko katika masoko ya dunia hupangwa na wakubwa na wenye nguvu huko nje "ambako nchi masikini huwa kama mbilikimo anayefurukuta mikononi mwa pandikizi la jambazi!" (kama hapo juu: 93)

Kama nilivyotamka mwanzoni, ni muhimu tukakumbuka kwamba yabidi mwaka huu tuuchukulie kama ni mwaka wa kuwaenzi wahenga wetu waliopigana dhidi ya wakoloni kwa nia ya kulinda hadhi na heshima yetu wote. Katika hali ya sasa hivi, tuna mengi ya kujifunza kutokan na mapambano hayo, kubwa zaidi likiwa ni lile la nini maana ya uhuru na uzalendo wa KiafriKa.

Marejeo

Bates, M. (1957): "Tanganyika under British Administration", Ph D Thesis, Oxford University, Oxford.

Chachage, C.S.L. (1986): "Socialist Ideology and the Reality of Tanzania", Ph D Thesis, University of Glasgow, Glasgow.

Cliffe, L. (1972): "Nationalism and the Reaction to Enforced Agricultural Change in Tanganyika during Colonial Period", in L. Cliffe & J. Saul (eds), *Socialism in Tanzania,* Vol 1, East African Publishing House, Nairobi (1972)

Cliffe, L. & G.L. Cunningham (1973): "Ideology, Organization and Settlement Experience in Tanzania", in L. Cliffe & J. Saul (eds), *Socialism in Tanzania,* Vol 2, East African Publishing House, Nairobi (1973)

Coulson, A. (1982): *Tanzania: A Political Economy,* Clarendon Press, Oxford.

Friedland, W.H. (1969): Vuta Kamba: The Development of Trade Unions in Tanganyika, Hoover Institution Press, Stanford.

Gann, L.H. & P. Duignan (1977): *The Rulers of German East Africa 1884-1914,* Stanford university Press, California.

Illife, J. (1979): *A Modern History of Tanganyika,* Cambridge University Press, Cambridge.

Karioki, James (1979): *Tanzania's Human Revolution,* Pennysylivania State University Press, New York.

Kimambo, I.N. (1971): *Mbiru: Popular Protest in Colonial Tanganyika,* East African Publishing House, Nairobi.

Kirilo, Japhet & Earle Seaton (1967): *The Meru Land Case,* East African Publishing House, Nairobi.

Kjekshus, H. (1977): *Ecology Control and Economic Development in East African History: The Case of Tanganyika 1850-1950*, Heinemann, London.

Maguire, G.A. (1969): *Towards 'Uhuru' in Tanzania,* Cambridge University Press, Cambridge.

Mapolu, H. (1986): "The State and the Peasantry", katika, I.G. Shivji (mhariri), *The State and the Working People in Tanzania,* CODESRIA, Dakar, 1986.

Mbee, Gicha (1970): “Letter From Mbugwe, Tanzania”, katika Irving Leonard Mrkovitz (mhariri), *African Politics and Society,* Free Press, New York.

McHenry, Dean E. (1973): “The Utility of Compulsion in the Implementation of Agricultural Policies: A Case Study from Tanzania”, katika *Canadian Journal of Afrivcan Studies,* Juzuu VIII, Namba 2, 1973.

Nyerere, J.K. (1966): *Freedom and Unity/Uhuru na Umoja,* Oxford University Press, Dar es Salaam.

Nyerere, J.K. (1973): *Freedom and Development/Uhuru na Maendeleo,* Oxford University Press, Dar es Salaam.

Nyerere, J.K. (1974): *Binadamu na Maendeleo,* Oxford University Press, Nairobi.

Robert, S. (1966): *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini,* Nelson, London.

Tanzania, United Republic of (1982): *The Tanzania National Agricultural Policy*, Government Printer, Dar es Salaam.

Tanzania, United Republic of (1994): *Report of the Presidential Commission of Inquiry into Land Matters*: Vol I, Land Policy and Land Tenure Structure, Ministry of Land, Housing and Urban Development & Scandinavian Institute of African Studies, Uppsala.

Taylor, J.C. (1963): *Political Development of Tanganyika,* Stanford University Press, Stanford.

Wisner, B., A. Kassami & A. Nuwagata (1973): “Mbambara: The Long road to Ujamaa”, in L. Cliffe & J. Saul (eds), *Socialism in Tanzania,* Vol 2, East African Publishing House, Nairobi (1973)